

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**Mkuu Mstahiki wa Jeshi ni Yule Anayekataa Kuitegemea Marekani, Anatoa Nusrh kwa ajili ya  
Kusimamisha Tena Khilafah na Kuhamasisha Kuikomboa Kashmir Iliyokaliwa**

**(Imetafsiriwa)**

Jenerali Bajwa kwa sasa yuko jijini Washington, akifanya mikutano ya kuagana na mabwana zake. Ajenda yake ni kuhakikisha kwamba Pakistan inasalia ndani ya mtego wa utumwa wa Marekani baada yake, anapofanya mazungumzo thabiti pamoja na Pentagon na maafisa wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani. Nguzo ya heshima iliyoimarishwa iliandaliwa kwa ajili yake, ikitambua utumishi wake wa muda mrefu na wa kina kwa Marekani.

Ni changamoto kwa jeshi la Pakistan na wenye ushawishi mkubwa kujiondoa katika utumwa wa kikoloni, baada ya Jenerali Bajwa kuondoka. Watu wenye nguvu wa Pakistan lazima wadhamini mkuu mpya wa jeshi ambaye atalinda na kutumikia maslahi ya Pakistan na Waislamu. Ni lazima wazuie mlinzi mwingine wa maslahi ya Marekani katika eneo hilo, mithili ya Jenerali Bajwa.

Kwa mujibu wa Uislamu, mkuu wa majeshi ya Kiislamu lazima atoe Nusrh kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah. Ni lazima atoe Nusrh kwa chama ambacho kinaweza kutabikisha Uislamu kwa ukamilifu, kwa njia ya kimapinduzi. Ni wajibu, uliolazimishwa na Mwenyezi Mungu (swt) kwa uongozi wa kijeshi wa Pakistan, kupindua mfumo wa sasa wa serikali usio wa Kiislamu, ulioundwa na binadamu, wa kidemokrasia. Ni lazima ufunge vituo vya kijasusi vya makafiri wachokozi, wanaojifanya kama mabalozi, na hivyo kupofusha miundombinu yao ya kijasusi. Ni lazima ukabidhi mamlaka kwa uongozi wenye ikhlasi, utambuzi, utakaofungua minyororo ya wanajeshi kutoka kwenye kambi, na kuwapeleka katika Jihad katika Njia ya Mwenyezi Mungu (swt).

Ni wajibu wa uongozi wa kijeshi wa Pakistan kuikomboa Kashmir Inayokaliwa kwa mabavu, na kukomesha ukandamizaji wa dola ya Kibaniani, ambayo imewaua mashahidi zaidi ya laki moja ya wanaume, wanawake na watoto wa Kiislamu, kuwabaka maelfu ya wanawake wasafi wa Kiislamu, na kupoteza maelfu ya vijana kwa nguvu, na kuwalazimisha watoto wetu kuimba nyimbo za kidini za Kibaniani.

Vikosi vya kijeshi vya Pakistan ni zawadi ya heshima ya Umma wa Kiislamu. Uongozi wao ni wa warithi wa Saad bin Muadh (ra), Khalid bin Walid (ra), Salahuddin Ayyubi (rh) na Muhammad bin Qasim (rh). Inatarajiwa kutoka kwa vikosi hivi kuwa mujahidina wa Ufunguzi wa Hind na ukombozi wa Msikiti wa Al-Aqsa. Jeshi la Pakistan lazima liwe mlinzi wa Uislamu na Waislamu, jambo ambalo Umma wa Kiislamu unatazamia na kudai kutoka kwao.

**Enyi Wanajeshi wa Pakistan!** Songeni mbele kwa ajili ya mafanikio katika Dunya na Aakhira! Songeni katika Jihad katika Njia ya Mwenyezi Mungu! Hamasikeni kwa ajili ya ukombozi wa Msikiti wa Al-Aqsa na kutokomeza uvamizi wa Kiyahudi! Jitokezeni kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah, na utabikishaji mara moja na wa kina wa Shariah! Jitahidini kwa ajili ya Pepo na maisha ya starehe zisizokwisha ambayo Mwenyezi Mungu (swt) amewaahidi waja wake watiifu. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمُ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ]

**“Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.”** [Surah Al-Hashr 59:7].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**